# Mahusiano Mema Mtandaoni

Washiriki wataangazia vigezo vinavyojumuisha mahusiano mema na karimu, na jinsi tabia mtandaoni huchangia mahusiano mema na yasiyo mema. Washiriki pia watatathmini nafasi na changamoto kuhusu ushirikiano baina ya mitandao ya kijamii na mahusiano katika vikundi vyao vya wanarika na wajifunze jinsi ya kuendeleza utetezi miongoni mwao.

# Kutaja Misamiati ya Mahusiano kwa Kupaza sauti

## Sehemu ya Kwanza

**Mwingiliano wa Darasa**

Wakusanye washiriki katika mduara.

**Ambia Wanafunzi Wako**

Leo, ningependa kuzungumza kuhusu jinsi shughuli zetu mtandaoni huathiri wema wa mahusiano yetu. Tutazungumza pia kuhusu kile unachoweza kufanya ili uwe "mtetezi" wa watu wengine, na tutambue marafiki zetu wanapohitaji usaidizi kuhusiana na baadhi ya matatizo yaliyo kwenye mahusiano.

**Uliza Wanafunzi Wako**

Nani amesikia kuhusu misamiati "wasimama kando" au "watetezi"? Je, maneno haya yana maana gani kwako?

**Mwingiliano wa Darasa**

Sikiliza majibu 2-3.

**Ambia Wanafunzi Wako**

Kama ulivyopendekeza, msimama kando ni mtu anayeshuhudia aina fulani ya kitendo kikitokea. Leo, tunazungumzia kuhusu vitendo vinavyohusiana na mahusiano yasiyo mema/ yasiyo karimu. Mtetezi ni mtu ambaye hushughulikia jambo kwa kuchukua hatua nzuri – pengine kwa kuwasaidia waathiriwa, kusaidia kukomesha kitendo hicho, au kwa njia nyingine, kwa kutegemea hali yenyewe.

## Sehemu ya Pili

**Ambia Wanafunzi Wako**

Sasa hebu tuzungumzie kuhusu mahusiano: kwanza, tunapaswa kutambua kwamba "mahusiano" ni msamiati mpana. Kwa madhumuni yetu, tutafafanua "mahusiano" kuwa na maana ya muunganisho wowote baina ya wanarika. Kwa mfano, unaweza kuunganishwa na wanarika wako kama marafiki, watu mnaosoma nao pamoja au wanachama wa shughuli sawa mnayofanya nje ya shule (mfano, klabu ya filamu). Kila mara tunapozungumza kuhusu mahusiano mema, swali gumu huchipuka: "Je, maana hasa ya mahusiano mema ni nini?" Kila mtu ana mawazo tofauti kuhusu mada hii, na kuna majibu mengi mazuri.

Ili tuhakikishe kwamba tunaelewana, hebu tufikiri na tutaje kwa sauti maneno

yanayoweza kufafanua mahusiano mema – urafiki, watu tunaosoma pamoja, mahusiano mbalimbali! Tunafahamu kwamba wakati fulani mambo yanaweza kuharibika katika aina zote za mahusiano, kwa hivyo, hebu tuzungumze kuhusu tabia njema ambayo ni mahususi kwa kila aina.

Hebu tucheze mchezo mdogo. Tunavyozunguka, hebu kila mmoja aseme neno moja linalofafanua mahusiano mema. Nitaanza. Ninadhani mahusiano yanaweza kuwa _________________ (ya kusaidia, ya kutunza, karimu, n.k).

**Mwingiliano wa Darasa**

Nakili yale washiriki wanasema kwenye chati inayozunguka.

**Ambia Wanafunzi Wako**

Vyema sana! Asante kwa kuchangia! Hebu tuangalie maneno haya.

**Uliza Wanafunzi Wako**

Je, unakubaliana nao?

Je, una jambo lolote la ziada la kuongeza?

Kulingana na maneno haya, je, mtu anaweza kubuni sentensi moja linalofafanua mahusiano mema?

Elekeza kikundi katika kuunda ufafanuzi shirikishi wa mahusiano mema.

# Utalii wa Kichanja

## Sehemu ya Kwanza

**Mwingiliano wa Darasa**

Wapange washiriki katika jozi.

**Ambia Wanafunzi Wako**

Sasa kwa vile tuna orodha nzuri ya mambo tunayofikiri kuhusu tunapozungumza kuhusu 'mahusiano mema,' ni wakati wa kubadilisha tafakuri yetu kidogo na tuangalie mambo tuliyoyapitia wenyewe kuhusu mahusiano kwenye Intaneti.

**Mwingiliano wa Darasa**

Andika swali moja kutoka kwenye orodha iliyo hapa chini kwenye bango na utundike mabango sehemu mbalimbali chumbani.

Maswali Yanayowezekana kwenye Bango:

1. Je, wewe hutagusana na nani kupitia teknolojia?

2. Je wewe hutumia majukwaa, huduma au tovuti zipi unapotagusana na watu?

3. Je, Intaneti na teknolojia ya simu (kama vile kompyuta kibao au simu za mkononi) zimekupa nafasi kivipi za kuunda na kudumisha mahusiano mema?

4. Je, unaweza kuwasiliana vipi na watu kwa kutumia vifaa vya mkononi na kompyuta?

5. Je, ni changamoto zipi ambazo zinatokana na Intaneti na teknolojia ya simu katika kuunda/kudumisha mahusiano mema?

6. Je, ni sokomoko zipi za urafiki ambazo umeona au kupitia kwa sababu ya vitu vilivyochapishwa mtandaoni?

**Ambia Wanafunzi Wako**

Ninaenda kumpa kila mmoja vidokezo vya kubandika na kalamu. Kuna maswali mbalimbali kwenye mabango yaliyo chumbani. Nikikupa vifaa vyako, unaweza kusonga kote chumbani. Andika majibu yako chini kwenye vidokezo vya kubandika kisha uviweke kwenye mabango. Ikiwa una majibu zaidi ya moja kwa swali moja, nakili kila jibu kwenye kadi tofauti na uyaweke kwenye mabango. Una dakika 8. Furahia!

**Mwingiliano wa Darasa**

Kusanya mabango mwishoni mwa shughuli hii na ukusanye kikundi pamoja tena.

**Uliza Wanafunzi Wako**

Je, majibu yepi yanafanana kwa kila maswali haya?

Je, kuna mambo yoyote unayofikiri hayapo?

Je, kuna mambo maarufu unayotazama?

Je, teknolojia imebadilisha vipi mahusiano yako na marafiki zako?

Je, teknolojia imekurahisishia mambo au imekuwekea mambo yawe magumu? Kwa nini?

# Mjadala wa Mfano

## Mjadala

**Ambia Wanafunzi Wako**

Sasa tutajadili mfano fulani unaohusiana na teknolojia na mahusiano unaoitwa “kutuma ujumbe sana.”

Je, kuna yeyote anayefahamu “kutuma ujumbe sana” kuna maanisha nini?

**Mwingiliano wa Darasa**

Sikiliza majibu 2-3.

**Ambia Wanafunzi Wako**

Kutuma ujumbe sana ni pale ambapo mtu anatuma ujumbe mingi kwa mtu mwingine ambapo mwenzake analemewa.

**Uliza Wanafunzi Wako**

Je, kuna yeyote ambaye amepitia hali ya kutumiwa ujumbe mwingi zaidi?

Ikiwa wewe ndiye mtu aliyekuwa anapokea ujumbe huu, je unaweza kufanya nini? Kwa nini?

Ikiwa marafiki zako wangekuja kwako na wakuambie kwamba wanapitia hali sawa, je unaweza kuwapa ushauri upi? Je, unaweza kuchukua hatua? Je, ni aina zipi za hatua tofauti unazoweza kuchukua?

1. Fuatilia: Kuchukua hatua hizi kusaidia marafiki zako kunajulikana kama “utetezi.”

**Uliza Wanafunzi Wako**

Je, ni jambo gani linaweza kumzuia mtu kumtetea rafiki yake?

Hebu tuchukulie kwamba mmoja wa marafiki zako anauliza rafiki yake aache kumtumia ujumbe mwingi sana. Je, nini hufanyika ikiwa rafiki wake ataanza kuja nyumbani kwake kila mara, akisistiza kutaka kumwona? Tatizo linaonekana kuwa mbaya zaidi, linaloweza kutajwa kuwa “kuenea.” Je, ni ushauri upi unaoweza kumpa rafiki yako ikiwa tatizo litaenea?

Ikiwa tatizo hili litaenea, je unaweza kulishughulikia bado kama mtetezi jinsi ulivyofanya hapo nyuma? Je, unaweza kuchukua hatua zipi sasa za kuwa mtetezi?

**Ambia Wanafunzi Wako**

“Kutuma ujumbe wa maandishi sana” ni mfano mmoja tu wa hali ambapo teknolojia inaweza kuzuia kuwepo kwa mahusiano mema.

**Uliza Wanafunzi Wako**

Je, mifano mingine ni ipi?

Je, baadhi ya suluhu kwa matatizo haya ni yapi?

Je, mjadala huu kufikia sasa umetuambia nini kuhusu nafasi ya teknolojia katika mahusiano?

**Mwingiliano wa Darasa**

Elekeza mjadala kuhusu athari njema na mbaya ya teknolojia kwenye mahusiano.

# Upeo wa Shughuli

## Sehemu ya Kwanza

**Ambia Wanafunzi Wako**

Hebu tuangazie tabia mahususi katika mahusiano mema na yasiyo mema na mahali walipo katika upeo huo kuanzia mema hadi yasiyo mema.

Nitampa kila mmoja wenu kidokezo cha kubandika. Kwenye kidokezo hiki cha kubandika kuna shughuli inayofanyika katika mahusiano, kwa mfano "kumtumia mpendwa wako ujumbe saa 24, siku 7" au "kubadilishana manenosiri kwenye mitandao ya kijamii." Mara tu nikishakupa kidokezo cha kubandika, ningependa usimame na uende katika sehemu ya mbele ya chumba. Upande mmoja wa chumba ndipo tabia njema za mahusiano na katika sehemu nyingine kuna tabia zisizo njema za mahusiano.

Ukija, fikiria kuhusu jinsi tabia iliyo kwenye kadi ilivyo au isivyo njema na usimame kwenye foleni. Kwa mfano, ikiwa unaamini kwamba "kumtumia mpendwa wako ujumbe saa 24 siku 7" sio tabia njema sana ikilinganishwa na "kupenda na kushiriki upya kila kitu ambacho marafiki zako wanachapisha," basi simama karibu na sehemu ya isiyo njema.

**Mwingiliano wa Darasa**

Mada zilizopendekezwa kwenye kadi:

1. Kumtumia mpendwa wako saa 24 siku 7
2. Kubadilishana manenosiri kwenye mitandao ya kijamii
3. Kusoma ujumbe wa rafiki yako bila kibali chake
4. Kuzungumza na wageni / watu usiowafahamu vyema mtandaoni
5. Kuandika maoni yakifidhuli kwenye chapisho la mtu kwenye mitando ya kijamii
6. Kumtumia mtu unayempenda ujumbe wa "usiku mwema" au "asubuhi njema" (pengine kila siku)
7. Kuzungumza kuhusu mzozo uliokuwa nao na rafiki fhadharani kwenye jukwaa la mtandao wa kijamii
8. Kupenda na kushiriki kila kitu marafiki zako wanachapisha
9. Kuchapisha maudhui kwenye mitandao ya kijamii ukitumia akaunti ya rafiki yako

(ukitumia jina lake)

10. Kuhusisha marafiki kwenye picha kutoka kwenye sherehe
11. Kueneza umbeya kuhusu mwanafunzi mwenzako katika mtandao ya kijamii

Wakati washiriki wanaposimama na kujipanga, waulize kuhusu sababu zao za kusimama mahali wanaposimama na uwahimize washiriki kusonga ili wasimame popote pale ikiwa watajihisi kufanya hivyo.

Mara tu washiriki wakijipanga katika upeo, waulize waweke vidokezo vya kubandika kwenye sehemu ya mbele ya chumba kisha warudi nyuma ili waweze kuona upeo ule mzima.

**Mwingiliano wa Darasa**

Iwapo watafanya hivyo, washiriki wanaweza kujibu maswali mawili ya kwanza yaliyo hapa chini kupitia katika mjadala, kuliko kuyaandika kwenye vidokezo vya kubandika na kuviweka ukutani mbele ya chumba.

**Uliza Wanafunzi Wako**

Je, kuna tabia nyingine zisizo njema unayoweza kufikiri?

Je, kuna tabia nyingine njema unayoweza kufikiri?

Je, kuna utaratibu mmoja wa kupangwa kwa upeo huu? Kwa nini / kwa nini hawakufanya hivyo? Je, nyote mnakubali?

**Uliza Wanafunzi Wako**

Tunaweka tabia hizi mahususi kwenye upeo kuanzia njema hadi zisizo njema. Lakini, je, kunaweza kuwa na hali ambapo tabia njema hubadilika kuwa zisizo njema? Au vinginevyo? Je, hali hii inaweza kutokea wakati upi?

Ikiwa X ni tabia isiyo njema [chagua tabia mahususi ambazo washiriki waliweka karibu na sehemu ya upeo ya “njema”], unawezaje kusuluhisha hali hii?

Je, unaweza kuongea vipi na mtu ikiwa hupendi mambo wanayofanya?

# Kazi

## Sehemu ya Kwanza

**Ambia Wanafunzi Wako**

Tumezungumza sana leo kuhusu teknolojia na mahusiano. Kwa vile sasa tumekupa tafakuri, je unaweza kushiriki vipi yale uliyojifunza pamoja na wengine? Je, unaweza kuunda aina gani ya shughuli ili kuwahimiza wanarika wako ili wawe watetezi ikiwa wataona aina yoyote ya tabia mbaya katika mahusiano?

**Utoaji**

Wagawe washiriki katika makundi 3 au 4.

**Ambia Wanafunzi Wako**

Tuna mapendekezo mawili sasa lakini ikiwa una wazo tofauti, basi lilete! Una muda dakika 30:

1. Pendekezo #1: Unda mwongozo wa tukio linalowezekana kwa ajili ya watu walio shuleni kwako au jamii kuhusu nafasi ya teknolojia katika mahusiano. Tukio hili linaweza kuwa kuonyesha/kujadili Makala, kampeni kama vile “Wiki ya Kueneza Upendo,” au hata wasilisho! Toa mifano ya jinsi ungetumia mitandao ya kijamii kama vile Facebook au Twitter kutangaza tukio. Uko huru kuunda picha pamoja na (mfano michoro au meme, n.k) yako mtandaoni.

2. Pendekezo #2: Unda hadithi kuhusu mahusiano (mahusiano baina ya watoto wa familia moja au mahusiano baina ya marafiki shuleni) na jinsi mahusiano haya yanaweza kuathiriwa na mitandao ya kijamii. Unaweza kuigiza mchezo mfupi, kuunda picha (mfano, mchezo wa utani), au unakili mfano wa taarifa kwenye Facebook au mazungumzo kwenye Twitter. . .tuwe wabunifu!

## Sehemu ya Pili

**Utoaji**

Baada ya dakika 30, waulize wanakikundi washiriki yale waliyounda na uwahusishe katika mjadala ukitumia maswali yafuatayo.

**Uliza Wanafunzi Wako**

Je, unashughulikia mada gani? Je, unataka watu wajifunze nini kuhusu wazo lako?

Je, wazo hili litanufaisha vipi shule/jamii/marafiki zako?

Hadhira yako lengwa ni ipi?

Je, utatangaza vipi wazo lako kwa hadhira yako lengwa?

Je, unafikiri hadhira yako itahisi vipi?

# Tafakari ya Mwisho

## Uakisi

### Ambia Wanafunzi Wako

Tunatumahi kwamba nyote mmefikiria kuhusu mahusiano mema kwa kina zaidi haswa kuhusiana na jinsi teknolojia imebadilisha mambo. Pia tuliwataka mfikirie kuhusu njia za kuwahimiza marafiki zenu ku "tetea," au kujitetea weyewe na wengine wanapoona jambo wasilolipenda au jambo linalowavunja moyo.

### Uliza Wanafunzi Wako

Je, mlijifunza mambo kama yapi?

Je, shughuli uliyopenda zaidi ni ipi? Kwa nini?

Je, shughuli ambayo hukupenda sana ni ipi? Kwa nini?

Je, unaweza kutekeleza vipi mambo uliyojifunza au kufanya maishani mwako?

Je, unaweza kueleza vipi mambo uliyofanya kwa marafiki zako?

Je, jambo jipya au la kushangaza uliyojifunza ni lipi?

Je, una maswali mengine kuhusu mahusiano mema au yasiyo mema?

Rasilimali hii ya mafunzo inapatikana kwa Vijana na Vyombo vya Habari katika Kituo cha Berkman Klein kwa Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Berkman Klein chini ya leseni ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International, bora tu utoe sifa kwa Vijana na Vyombo vya Habari kama chanzo asili na ushiriki kazi nyingine za ziada chini ya masharti yayo hayo.Hizi pamoja na rasilimali nyingine za mafunzo pia zinapatikana mtandaoni kwenye Jukwaa la Rasilimali ya Kusoma na Kuandika Kidijitali la Berkman Klein.